Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.46, - 2025

wizara_elimuTanzania  wizara_elimuTz  www.facebook/moestvt.com  www.wyestu.blogspot.com  www.moe.go.tz  ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






# PROF. MKENDA NA MHE. WANU AMEIR KUENDELEZA MAGEUZI YA ELIMU NCHINI

- KAZI NA UTU TUNASONGA MBELE -




**BODI YA UHARIRI**

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Lucas Haule
Miriam Olomy
Fradius Mugoa
Elizabeth Marwa
Dionice Lukweme
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

# ELIMU KWA WOTE, BILA KUACHA MTU NYUMA

Mnamo Novemba 12, 2025, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilizindua Mpango wa Utekelezaji wa Mwongozo wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo. Hatua hii ya kihistoria inalenga kuhakikisha kila mtoto nchini anapata fursa ya kuendelea na elimu, bila kujali changamoto alizokutana nazo, na hivyo kuimarisha usawa wa upatikanaji wa elimu kwa wote.

Uzinduzi huu unaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kutekeleza sera za elimu kwa vitendo na kuondoa vikwazo vinavyowazuia watoto kuendelea na masomo. Mpango huu pia unatoa dira ya kitaifa kwa wadau wa elimu, ukisisitiza kuwa changamoto kama ujauzito, mazingira magumu ya kifamilia au sababu nyingine hazipaswi kuwa mwisho wa ndoto za kielimu, bali ni nafasi ya kuwasaidia kurejea shuleni na kujijengea mustakabali bora huku wakilinda haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Aidha, taarifa ya utafiti iliyozinduliwa sambamba na mpango huu inatoa ushahidi wa matokeo chanya, zaidi ya wanafunzi wa kike 13,000 na wa kiume 17,000 wameweza kurejea shuleni na kuendelea na masomo. Hii ni takwimu inayothibitisha kuwa juhudi za urejeshaji hazibaki kwenye karatasi pekee, bali zinagusa maisha halisi ya watoto na familia zao.

Ushirikiano wa Serikali na wadau kama Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) na UNICEF unaonesha wazi kuwa mafanikio ya sekta ya elimu yanahitaji nguvu ya pamoja. Ili kwa pamoja tuweze kulinda mustakabali wa watoto wetu wa kielimu.

Tunaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza mageuzi ya elimu kuhakikisha kila mtoto anapata nafasi ya kujifunza na kufikia ndoto zake. Ni wajibu wa jamii nzima kuunga mkono mpango huu ili kuimarisha usawa wa fursa za elimu, na kujenga kizazi chenye maarifa na ujuzi wa kuchangia maendeleo ya taifa.



Ukaribisho >

# PROF. MKENDA NA MHE. WANU AMEIR KUENDELEZA MAGEUZI YA ELIMU NCHINI



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, amesisitiza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga kuhakikisha elimu inayotolewa inawawezesha vijana kupata maarifa, stadi stahiki na ujuzi ili waweze kujiajiri na kushindana katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi.

Prof. Mkenda amesema hayo Novemba 18, 2025 jijini Dodoma, akizungumza na Watumishi wa Wizara hiyo, akisisitiza kuwa Serikali chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu, yanayolenga kutoa elimu bora, kuongeza fursa za ujifunzaji ili kuendana na mahitaji ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

Waziri Mkenda ameongeza kuwa Wizara itasimamia kikamilifu elimu katika ngazi mbalimbali na kuweka mkazo katika mafunzo ya amali.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Wanu Hafidh Ameir ameahidi ushirikiano katika kufanikisha mageuzi hayo na amehimiza kuendeleza utamaduni wa ushirikiano na weledi katika kazi ili kuhakikisha malengo ya Serikali ya kutoa elimu bora kwa wote yanafanikiwa.

Mhe. Wanu na Prof. Mkenda wamepokelewa rasmi katika ofisi za Wizara, ambapo watumishi wamewafurahia Viongozi hao na wameonesha ari ya kushirikiana katika safari ya mageuzi ya elimu.



Kuwarejesha Shule >

# DKT. OMAR AZINDUA MPANGO WA UTEKELEZAJI MWONGOZO WA KUWAREJESHA SHULE WALIOKATIZA MASOMO

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Mohamed Omar, Novemba 12, 2025, jijini Dar es Salaam, amezindua Mpango wa Utekelezaji Mwongozo wa kuwarejesha shule wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali, hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa elimu inapatikana kwa kila mtoto nchini.

Dkt. Omar ameeleza kuwa Mpango huo ni muhimu na utatoa dira kwa Serikali na wadau elimu katika kutekeleza kikamilifu sera ya elimu na Mwongozo wa urejeshaji ili kuhakikisha kuwa watoto wote, bila kujali changamoto walizokutana nazo, wanapata nafasi ya kuendelea na masomo yao.

"Watoto wetu wa kike na wa kiume, wanapokatisha masomo, si mwisho wa maisha yao, kuna fursa zaidi ya elimu ili kufikia malengo yao na waweze changia maendeleo ya taifa kwa ujumla" amesisitiza Dkt. Omar.

Aidha ameupongeza Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) pamoja na wadau mbalimbali wa elimu katika kufanikisha utekelezaji wa mkakati huo unaolenga kutoa fursa sawa kwa watoto wote katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari.

Katika hatua nyingine Dkt. Omar pia amezindua taarifa ya utafiti uliofanyika juu ya utekelezaji Mwongozo wa urejeaji kwa kundi moja la wanafunzi wa kike waliokatisha masomo kutokana na ujaouzito.

Taarifa hiyo inaelezea mafanikio makubwa ambayo yamewezesha wanafunzi wa **kike zaidi 13,000 na wa kiume 17,000** kurejea kuendelea na masomo.

Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Bi. Martha Makala, ameipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuongeza wigo wa ushirikiano na wadau mbalimbali wa elimu ambao umeimarisha mahusiano na kuchochea utekelezaji wa kazi mbalimbali.




Amesema kuwa ushirikiano huu, umesaidia kutumia vema rasilimali zinazopatikana kutekeleza mikakati mbalimbali kuwezesha elimu bora kwa watoto wetu.



Elimu ya Ufundi >

# CHUO CHA UFUNDI DODOMA KITOVU CHA ELIMU YA UFUNDI NCHINI - MHE. WANU

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, amesema uanzishwaji wa Chuo cha Ufundi Dodoma (DTC) ni hatua kubwa ya Serikali katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Akizungumza Novemba 27, 2025, Naibu Waziri amebainisha kuwa chuo hicho kimekusudiwa kuwa kitovu cha utoaji wa elimu ya ufundi bora nchini, kitakachowawezesha vijana kupata ujuzi na stadi za kazi zitakazowaandaa kushiriki kikamilifu katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi.

Aidha, amesisitiza kuwa lengo kuu la Serikali ni kuhakikisha taifa linakuwa na nguvu kazi yenye ujuzi, ubunifu na ushindani wa kimataifa.

Naye Naibu Katibu, Dkt. Hussein Mohamed Omar, amesema awamu ya kwanza ya ujenzi katika Chuo hicho, Serikali imejenga madarasa, mabweni, ofisi, karakana pamoja na ununuzi wa samani zote muhimu ili kuhakikisha mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia.



Aidha, Dkt. Omar amesisitiza dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuendeleza ujuzi nchini na kuwa Wizara itaendelea kukisaidia chuo hicho ili kiweze kujiendesha kwa ufanisi na kutoa mafunzo ya ufundi stadi yatakayo wawezesha wanachuo kupata ujuzi wa vitendo, kujiajiri na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

> *"Lengo kuu la Serikali ni kuhakikisha taifa linakuwa na nguvu kazi yenye ujuzi, ubunifu na ushindani wa kimataifa.*



Elimu ya Biashara >

# CBE YATAKIWA KUANZISHA KOZI ZA WALIMU WA BIASHARA




> **"CBE imefanya tafiti 418 na kuchapisha machapisho 447 ndani ya miaka mitano**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, ametoa wito kwa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuanzisha kozi maalum za muda mfupi na mrefu za Elimu ya Biashara.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Sita wa Kitaaluma wa chuo hicho Novemba 12, 2025 Jijini Dodoma, Prof. Nombo amesema hatua hiyo ni muhimu kwa ajili ya kuzalisha walimu wa kufundisha somo la Biashara, ambalo sasa ni la lazima kwa wanafunzi wote kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, toleo la 2023.

Prof. Nombo ameipongeza CBE kwa mafanikio ya kitaaluma, ikiwemo kushika nafasi ya nane kati ya vyuo 47 vya elimu ya juu nchini kwa mujibu wa AD Scientific Index. Alisisitiza kuwa mafanikio hayo ni kielelezo cha dhamira ya chuo katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya viwanda na biashara.

Aidha, ameeleza kuwa **CBE imefanya tafiti 418 na kuchapisha machapisho 447 ndani ya miaka mitano,** akisisitiza umuhimu wa matokeo hayo kufikishwa kwa wananchi kwa lugha rahisi na inayoeleweka huku akitoa rai kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali.



Amesisitiza kuwa vyuo vya elimu ya juu vina jukumu la kuhakikisha matokeo ya tafiti yanawafikia wananchi wa kawaida kwa lugha rahisi na inayoeleweka. Ametoa rai kwa vyuo vingine nchini kuiga mfano wa CBE kwa kuandaa mikutano ya kitaaluma kama huo, kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kuendeleza tafiti na kupanua wigo wa maarifa katika sekta mbalimbali.

Ameeleza kuwa tafiti ni kiini cha mageuzi ya Taifa, na ushirikiano kati ya vyuo, Serikali na sekta binafsi ni muhimu ili kuhakikisha matokeo ya tafiti yanachochea maendeleo jumuishi.

Mkutano huo wa kitaaluma umejadili masuala muhimu yanayolenga kuimarisha ustahimilivu wa uchumi na biashara kwa maendeleo jumuishi. Mada zilizotolewa zinahusu uchumi wa kimataifa, ujumuishaji wa kifedha, teknolojia na ubunifu, usimamizi wa mnyororo wa ugavi, soko la ajira, na siasa za kikanda na umehudhuriwa na viongozi wa Serikali.

Mageuzi ya Elimu >

# TUSHIRIKIANE KUTEKELEZA MAGEUZI YA ELIMU – PROF. MKENDA

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa mageuzi ya elimu ni muhimu sana kwa taifa, hivyo tunalazimika kuyatekeleza ili kuandaa vijana wetu kukabiliana na changamoto za kiuchumi na kutumia fursa za teknolojia kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali Nchini.

Prof. Mkenda amesema hayo Novemba 27, 2025 jijini Dodoma akifunga Mkutano wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA), akisisitiza kuwa katika moyo wa mageuzi ya elimu, ni muhimu kuwandaa vijana wetu ili waendane na mabadiliko ya teknolojia na mazingira ya kidigitali.

"Ili kuwaandaa vijana kwa soko la ajira na kukabiliana na changamoto za utandawazi, tushirikiane kutekeleza mageuzi na tuwekeze kwenye sayansi na teknolojia" amesema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda amesema kuwa, katika kutekeleza Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, pamoja na mambo mengine Wizara inafanya maandalizi kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na elimu ya sekondari hatua ya chini mwaka 2028.

Aidha amesema kuwa Serikali inatambua mchango wa TAPSHA katika maendeleo ya elimu, hivyo amesisitiza chombo hicho kulinda familia ya walimu. Aidha amewapongeza walimu wote Nchini kwa kazi nzuri wanazofanya.

Akimwakilisha Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI Ndug. Adolf Ndunguru, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Dkt. Emmanuel Shindika, amesema kuwa Mkutano huo umekuwa jukwaa muhimu la kutathmini masuala mbalimbali ya kielimu na kuweka mikakati madhubuti ya utekelezaji wa Mtaala Ulioboreshwa.

Ameongeza kuwa majadiliano yaliyofanyika yameongeza uelewa na kuimarisha ushirikiano katika kuboresha elimu ya msingi nchini.



> "*Mtaala Ulioboreshwa Unazingatia Elimu bora ujuzi na ubunifu kwa maendeleo ya taifa*

Naye, Mwenyekiti wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi nchini Tanzania (TAPSHA) Bi. Rehema Ramole ameipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali katika kutekeleza mageuzi ya elimu ikiwemo pamoja na kuendelea kuboresha maslahi ya Walimu, kwani wanaendelea kupandishwa madaraja.

Mkutano huo umeongozwa na kaulimbiu inayosema: **Mtaala Ulioboreshwa kwa Elimu Bora: Ujuzi na Ubunifu kwa Maendeleo Endelevu ya Taifa.**



Mradi wa HEET >

# SERIKALI YAIMARISHA UJENZI WA KAMPASI ZA VYUO VIKUU NCHINI - PROF. MUSHI

Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa kukamilisha kwa wakati ujenzi wa kampasi 16 katika mikoa isiyo na vyuo vikuu, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya juu kwa vijana nchini.

Kauli hiyo imetolewa Novemba 17, 2025 jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi, katika kikao cha pamoja kati ya Wizara na Benki ya Dunia.

Prof. Mushi ameeleza kuwa miundombinu hiyo itakamilishwa kwa wakati ikiwa na Vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili ifikapo mwaka 2026 zianze kutumika kikamilifu, ili kuimarisha ujuzi wa kisayansi na kiufundi, na kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia rasilimali watu wenye ujuzi.

Benki ya Dunia, ambayo ni mshirika mkuu wa utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), imeahidi kuendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa ufanisi. Benki hiyo imesisitiza umuhimu wa usimamizi makini wa rasilimali ili kuhakikisha matokeo chanya kwa taifa.



Prof. Daniel Mushi
Naibu KAtibu Mkuu Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu

Sambamba na kikao hicho, Novemba 18, 2025 watekelezaji wa mradi wa HEET kutoka taasisi mbalimbali za elimu ya juu pamoja na Benki ya Dunia wamekutana kufanya tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo.

Aidha, wadau wamejadili namna mradi unavyoweza kuendelea kuleta matokeo ya kudumu kwa taifa kupitia mageuzi ya kiuchumi yanayotokana na elimu ya juu, ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wataalamu, kuimarisha ubora wa elimu na kuongeza ushindani wa rasilimali watu katika soko la ajira.



Lishe kwa Wanafunzi >

# RAI KWA WADAU KUBORESHA LISHE KWA WANAFUNZI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa wito kwa mashirika ya kimataifa na wadau wa maendeleo kuongeza ushirikiano katika kuboresha miradi ya chakula na lishe shuleni, ili kuhakikisha watoto wanapata afya bora na mazingira rafiki ya kujifunzia.

Rai hiyo imetolewa Disemba Mosi, 2025 jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Msaidizi wa Uendelezaji Sera za Elimu Msingi, Victor Bwindiki, kupitia kikao cha wadau wa mpango wa chakula shuleni. Kikao hicho kimetoa nafasi ya kubadilishana uzoefu, kujadili mafanikio na changamoto, pamoja na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha utoaji wa chakula mashuleni.

Aidha, washiriki wamewasilisha mbinu mbalimbali katika kuwezesha utekelezaji wa mpango wa chakula shuleni, pamoja na masomo yaliyopatikana kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Lishe, VVU na Mipango ya Shuleni kutoka Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP) Bi. Vera Kwara, amewashukuru wadau kwa mchango wao katika kuimarisha mpango huo muhimu kwa mustakabali wa elimu nchini.

> *“Wito kwa mashirika ya kimataifa na wadau wa maendeleo kuongeza ushirikiano katika kuboresha miradi ya chakula na lishe shuleni*



**Mhe. Victor Bwindiki**
Mkurugenzi Msaidizi wa uendelezaji Sera za Elimu Msingi

“Kwa baadhi ya watoto, mlo wa shule ndio chakula chenye lishe kamili wanachokipata kwa siku. Hivyo kuongeza utofauti wa vyakula, hususan vyenye protini na virutubisho, ni hatua muhimu,” amesema.



Usimamizi wa Vitabu >

# MFUMO WA UANDAAJI NA USIMAMIZI WA VITABU VYA KIADA WABORESHWA



**Mhe. Dkt. Joyce Sigalla**
Kaimu Mkurugenzi Msaidizi uendelezaji Sera ya Elimu ya Msingi

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza kuboresha Rasimu ya Kiunzi cha Uandaaji, Uchapaji, Uzalishaji, Usambazaji, Uhifadhi, Utunzaji na Matumizi ya Vitabu vya Kiada nchini.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao maalum kilichofanyika Morogoro, Novemba 18, 2025 kwa niaba ya Kamishna wa Elimu, Dkt. Joyce Sigalla, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Uendelezaji Sera Elimu ya Msingi alisema hatua hiyo ni sehemu ya mageuzi makubwa yanayoendelea katika sekta ya elimu.

Mageuzi hayo yanajumuisha Maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 (Toleo la 2023), Mabadiliko ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP III 2025/26–2029/30).

Dkt. Sigalla alieleza kuwa lengo kuu ni kujadili na kuboresha rasimu ya kiunzi kitakachoweka mfumo mmoja wa kitaifa katika mnyororo mzima wa kitabu, kuanzia uandishi na uhakiki wa kitaaluma hadi usambazaji, utunzaji na matumizi shuleni.

Aidha, kikao hicho kimewakutanisha wadau muhimu kutoka TAMISEMI, Taasisi ya Elimu Tanzania, Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, sekta binafsi na taasisi nyingine ili kuhakikisha mfumo unaojadiliwa una uhalisia, unatekelezeka, na unaweza kutatua changamoto zilizopo.



> **“*kuboresha Rasimu ya Kiunzi cha Uandaaji, Uchapaji, Uzalishaji, Usambazaji, Uhifadhi, Utunzaji na Matumizi ya Vitabu vya Kiada nchini.*”**

# MAGEUZI YA KIDIJITALI KWENYE ELIMU NI JUMUISHI NA ENDELEVU



> "Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa mabadiliko ya kidijitali katika sekta ya elimu yanakuwa jumuishi, shirikishi na endelevu.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Mohamed Omar amesema Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa mabadiliko ya kidijitali katika sekta ya elimu yanakuwa jumuishi, shirikishi na endelevu.

Dkt. Hussein ameyasema hayo Novemba 17, 2025 jijini Dodoma wakati akiongoza kikao cha majadiliano kuhusu muunganiko wa Mpango wa Msingitek na miradi mingine ya kitaifa inayotekelezwa katika elimu ya msingi, kikilenga kuongeza ufanisi na kuepuka urudufu wa juhudi.

Ameeleza kuwa Mpango wa Msingitek unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na wadau wa maendeleo, wakiwemo Imagine Worldwide, ambao wanatoa mchango wa kitaalamu na kifedha ikijumuisha vifaa vya TEHAMA, mafunzo kwa walimu pamoja na ushiriki katika ufuatiliaji wa matokeo ya utekelezaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Imagine Worldwide, Dkt. Jacqueline Mgumia, ambaye ni mtekelezaji wa mpango wa Msingitek, amewasilisha dira ya utekelezaji unaolenga kutumia TEHAMA kuimarisha ujifunzaji wa wanafunzi kwa zaidi ya shule elfu moja.

Amesisitiza umuhimu wa kuwepo kwa mawasiliano ya karibu miongoni mwa wadau ili kuhakikisha utekelezaji unakwenda sambamba na malengo ya kitaifa na vipaumbele vya Serikali.



# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi,
Muhimbili (MUHAS),
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius
Kambarage Nyerere,
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
**27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,**
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz

**- KAZI NA UTU TUNASONGA MBELE -**